# Zati inatafuta mbinu ya kukuza biashara ili kuinua uchumi Z'bar




**Mipango ya Taifa lolote ni ustawi wa uchumi wenye tija kwa maendeleo ya Taifa na wananchi wake lakini inapokuwa hakuna mipango mizuri ya kodi, matarajio hayo yatagonga mwamba**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Jumuiya ya wawekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (Zati) wamepokea Dola 52,500 za Marekani ili kutafiti mfumo wa kodi kwa lengo la kubaini kasoro zilizopo na kutoa mapendekezo ya uboreshaji kwa Serikali.

Fedha hizo zilizotolewa na Taasisi ya BEST- Dialogue ili kuisaidia sekta ya utalii visiwani Zanzibar kuondokana na mifumo mibaya ya kodi iliyopo sasa.

Zati wanaamini kuwa kwa kuboresha mfumo wa kodi visiwani humo kutasaidia kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara, kutasaidia kuhamasisha ulipaji kodi hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na upatikanaji wa ajira.

Mwenyekiti wa Zati, Omar Said Shaaban anaamini kuwa ulipaji kodi ni muhimu katika kuiwezesha Serikali kutoa huduma za msingi ambazo zinasaidia kukuza biashara lakini kodi ikiwa kubwa inachangia kudidimiza biashara na kuweka mazingira magumu ya kibiashara.

Ripoti iliyotolewa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na International Finance Corporation mwaka 2010, iitwayo Doing Business in Zanzibar Report imeiweka Zanzibar katika nafasi ya 155 kati ya 183 katika kuwa na mazingira bora ya biashara.

Wakati huo huo, Tanzania Bara imeshika nafasi ya 131 katika utafiti huo.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa katika mji wa Zanzibar kampuni ya kati inafanya malipo tofauti tofauti 48, inalipa asilimia 40.8 ya faida yake kama kodi na inatumia saa 158 kwa mwaka kushughulikia masuala ya ulipaji kodi kwa hiari.

Muda huo unajumuisha saa 26 kufanya mchakato wa kulipa kodi ya mapato (Corporate income tax), saa 60 katika kushughulikia kodi za wafanyakazi na saa 72 kushughulikia Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Ripoti inaeleza kwamba Visiwa vya Maldives ndivyo vinaongoza duniani kwa kuwa na kiwango kidogo zaidi cha kodi.

Biashara visiwani humo hutakiwa kulipa one single property-transfer tax payment kwa mwaka, ambayo huwa ni asilimia 9.1 ya faida.

Tangu mwaka jana Zati wamekuwa wakiiomba Serikali kufanya marekebisho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ili kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara visiwani humo.

Shaaban alieleza kuwa Zati inampango wa kuwasiliana (consult) na wadau wa utalii toka serikalini na sekta binafsi kutafiti na kuandaa mapendekezo ya mfumo bora wa kodi kabla ya kuyawasilisha serikalini.

"Ripoti itaeleza matokeo ya utafiti huo  na mapendekezo kwa lengo la kuhamasisha maboresho katika mfumo wa kodi na hivyo kuboresha mazingira ya biashara ambayo yatahamasisha watu kulipa kodi kwa hiari, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza imani kwa wawekezaji," anasema Shaaban.

Shaaban anaeleza kuwa mwaka 2013 Zati ilikutana na Rais na kubainishiwa kuwa ukuaji wa sekta ya utalii imezipita sekta zingine zote.

> **"Ripoti itaeleza matokeo ya utafiti huo na mapendekezo kwa lengo la kuhamasisha maboresho katika mfumo wa kodi na hivyo kuboresha mazingira ya biashara ambayo yatahamasisha watu kulipa kodi kwa hiari, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza imani kwa wawekezaj."**
>
> Omar Said Shaaban

Katika kipindi cha miaka kumi kati ya mwaka 2000 na 2012 sekta ya utalii visiwani Zanzibar ilikuwa kwa wastani wa asilimia 6.8 kwa mwaka.

"Matokeo ya ukuaji huo, mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa ulikuwa kutoka tarakimu moja mwaka 2004 hadi kufikia zaidi ya asilimia 27 mwaka 2012," alisema Shaaban.

Zati inaamini kuwa maboresho katika mfumo wa kodi visiwani humo siyo utasaidia kuboresha mazingira ya biashara bali utachochea ukuaji wa uchumi.

Uchumi ukikua utasaidia kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa na kuongeza uwekezaji wa kigeni wa moja kwa moja (Foreign Direct Investment).

Pia, ukuaji wa uchumi utasaidia kukuza soko la ajira katika sekta ya utalii na maeneo yanayohusiana na utalii.

Zati imeambia Mwananchi kuwa kuanzia mwezi wa kwanza hadi wa saba mwaka 2014 idadi ya watalii waliotembelea Zanzibar iliongezeka kwa asilimia 13.96 ikilinganisha na kipindi kama hicho mwaka 2013.

Jumla ya watalii 106,390 walitembelea visiwani humo ukilinganisha na 93,351 waliotembelea visiwa hivyo mwaka 2013.

Kwa mujibu wa Zati kuanzia mwezi wa kwanza hadi wa saba mwaka 2014 Zanzibar ilipokea watalii 77,450 kupitia viwanja vya ndege na ilipokea watalii 28,940 kupitia bandari.

Zanzibar pia ilipokea watalii wa ndani 49,929 na kufanya jumla ya watalii wa ndani hadi sasa kufikia 156,319.

Ripoti ya Benki ya Tanzania inaonyesha kuwa huduma za akaunti zilirekodi ziada ya Dola 81.1 milioni katika kipindi cha mwaka unaoishia Januari 2015.

Kipindi kama hicho mwaka 2014 huduma za akaunti zilirekodi  Dola 77 milioni.

"Ziada hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na ongezeko la mapato katika shughuli zinazoendana na utalii," inasema ripoti hiyo.

**Habari zaidi**

Zati ni taasisi isiyo ya kiserikali, kidini wala kisiasa iliyoanzishwa ili kuwakilisha matakwa ya wawekezaji wote wa utalii visiwani Zanzibar.

Zati inalengo la kushawishi ili kuwe na sekta ya utalii iliyo endelevu na ya kitaaluma inayofuata maadili ya hali ya juu ya utendaji kazi. Zati inafanya kazi na taasisi za Serikali kufikia malengo hayo.

Zati ipo mstari wa mbele katika kuunganisha ubia kati ya Serikali na mashirika binafsi kujadiliana na kushawishi masuala ya kiutalii na kutangaza vivutio vilivyopo Zanzibar.

BEST–Dialogue ni taasisi inayotoa misaada ya kifedha ili kusaidia taasisi na mashirika binafsi kuandaa mazingira bora ya biashara nchini Tanzania.

Pesa zinazotolewa na BEST-Dialogue zinasaidia taasisi binafsi kufanikisha mazungumzo kati ya taasisi hizo na Serikali yanayosaidia kurekebisha sera, sheria na kanuni mbalimbali kwa lengo la kuboresha sekta ya utalii visiwani humo.

Zanzibar inashika nafasi ya 155 kati ya nchi 183 duniani katika kuwa na mazingira bora ya ufanyaji biashara. Hii ni kutokana na ripoti ya ufanyaji biashara ya mwaka 2010 (Doing business in Zanzibar 2010 report).

***Kila Alhamisi katika gazeti la Mwananchi***

***Ukurasa wa Urahisi wa Kufanya Biashara umerudi katika Jarida la Uchumi, gazeti la Mwananchi kila Alhamisi. Lengo lake ni kusaidia juhudi za kuboresha mazingira ya ufanyaji wa biashara Tanzania.***

***Kwa mrejesho tutumie ujumbe mfupi wa maneno kupitia 0786240172. Washiriki wanne, watapewa muda wa maongezi wa Sh10,000.***

BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo